

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO**

Mongola shule ya Sekondari  
S.L.P 125  
Morogoro  
Tel: 0786594040

Kumb . No MSS/S.2229/J/2019

16/12/2021

MLEZI /MZAIZI WA.....

**YAH: TAARIFA YA KUCHAGULIWA KUJIUNGA  
KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.**

1. Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kuijunga kidato cha **KWANZA katika shule ya Sekondari Mongola** iliyopo Wilaya ya Mvomero, Tarafa ya Mlali, katika kata ya **Mzumbe**, Kijiji cha **Changarawe**.

Natumia fursa hii kukupongeza na kukupatia maagizo muhimu ya kujiunga na shule. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shulen 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti tarehe 30/01/2021.

**KARIBU SANA MONGOLA SEKONDARI.**

(a) **SCHOOL MOTO:** “EDUCATION FOR LIFE EXCELLENCE”

(b) **SCHOOL VISION:**

“To become among the best schools which will provide students with competent and suitable knowledge to enable them to join high learning institutions, obtain employment and hence achieve better living standard.”

**2.1 MAHITAJI YA LAZIMA**

**SARE ZA SHULE**

**(A) WAVULANA**

- Shati jeupe tetroni lenye mikono mifupi (mawili)
- Suruali yenye marinda na tun-up rangi ya kijani isiyo ya kubana(Mbili) chini upana wa nchi 18 ikiwa tofauti hatapokelewa[Rangi ya kijani kama ya shule ya morogoro sekondari]
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visivyo na kisigino kirefu (Jozi mbili)
- Soksi ndefu nyeusi
- T.shirt rangi ya dark blue
- Sweta isiyo na ukosi ya rangi ya kijani yenye mikono mirefu
- Kila mwanafunzi aje na picha tatu (03) za passport size

**NB**

- Sare yenye rangi ya mitindo na mishono tofauti na taratibu za shule hazitapokelewa
- Suruali ivaliwe na mkanda mweusi usio na kifungio kikubwa au alama au maandishi makubwa
- Suruali zinapatikana shulen kwa bei ya tsh 18000/=

**(B) WASICHANA**

- Blauzi nyeupe tetroni za mikono mifupi (2)

- Sketi ya rangi ya kijani mshono wa rinda box. (mbili) ivuke vifundo viwili nya miguu, ikiwa tofauti na hapo mtoto wako hatopokelewa [Rangi ya kijani ifanane na ya shule ya Morogoro sekondari]
- Viatu vyeusi nya ngozi na visivyo na kisigino kirefu na vyenye kamba
- Sweta isiyo na ukosi ya rangi ya kijani
- T.shirt rangi ya Dark Blue.
- Hijabu zinaruhuswa kwa wasichana kufuatana na taratibu za hijabu ( hijabu ivuke vifundo viwili nya mikono na iwe ya kushonwa na sio ya kununua dukani.
- Hatutapokea sare zisizozingatia maadili.
- Kila mtoto aje na picha tatu (03) za passport size

## **2.0 VIFAA VYA KUJIFUNZIA NA USAFI (MZAIZI/MLEZI ANUNUE)**

- Madaftari makubwa 12 yenye kurasa 48 au counter book 11.
- Mkebe (mathematical set) moja (01)
- Rula ndefu, kalamu na penseli.
- Begi la kubebea madaftari (mfuko wa Rambo hauruhusiwi)
- Vifaa nya usafi – aje na fagio la chelewa kwa ajili ya usafi

## **3.0 HATI YA LAZIMA**

Hati zifuatazo zikamilishwe na kila mwanafunzi aje nazo shuleni kwa ajili ya kumbukumbu zake:

- Cheti cha kuzaliwa –Nakala moja (01)
- Fomu ya hospitali (Request for Medical Examination). Fomu zimeambatanishwa LAZIMA mwanafunzi apimwe na Mganga wa Serikali na kujaza fomu hiyo kikamilifu

**4.0 Mahitaji Muhimu:** Kupungukiwa au kukosa baadhi ya mahitaji hayo SIYO kigezo cha mwanafunzi kutokuripoti shuleni. Kama kuna tatizo lolote au unahitaji ufanuzi njoo tuzungumze.

- 1) Siku ya kuripoti shuleni ni tarehe 06/01/2021. lazima mzazi/mlezi amlete mtoto wake. Fika moja kwa moja ofisi ya Mkuu wa shule / Makamu Mkuu wa Shule ili kumuandikisha mtoto.
- 2) Kwa wale watakaowapeleka watoto wao shule binafsi (private) watatakiwa Kutoa taarifa shuleni au kwa mtendaji wa kijiji kwa maandishi na kuleta shuleni nakala ya taarifa ya uhamisho kwa njia ya mfumo, hii itasaidia kupata takwimu za wanafunzi wasioripoti/wasiopelekwa shuleni, na hatimaye kuwezesha serikali za kata/ vijiji kufuatilia wanafunzi waliofaulu na kuwa Mitaani.

## **MWISHO**

Ni matumaini yetu kuwa kila mwanafunzi na mzazi /mlezi atafuata na kuzingatia mambo yote yaliyoorodheshwa hapo juu kwa lengo la kufanikishwa malezi na utoaji wa elimu bora hapa Mongola Sekondari.

.....  
D . P DOTO.

MKUU WA SHULE.